




Tanzania Media
Women's Association

TAMWANites Konnect

Issue No. 008 - August, 2019



VISION

A peaceful Tanzania society which respects human rights from a gender perspective.

MISSION

To advocate for women and children's rights for cultural, policy and legal changes/ transformations in the society through the use of media.

Marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani ni Muhimu

Serikali inayoamini katika mabadiliko chanya, lazima ipendwe na wananchi wake. Jambo ambalo, wananchi wanalipigia kelele kila mara kuwa lina madhara ndani na inatakiwa ifanyiwe marekebisho kisheria, tambua kuwa wamechoka na jambo hilo, ndiyo maana wanalipigia kelele. Sheria za usalama barabarani ya mwaka 1973, inapigiwa kelele na wadau wengi wa maendeleo husasani wale wanaosimamia usalama barabarani. Kilio kilikuwa kikubwa dhidi ya sheria hii ambayo wadau hao, wanaona ina mapungufu mengi ya kiutendaji.

Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola (MB), akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20, namnukuu". Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 Jeshi litaendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, utaratibu wa kupata ridhaa ya Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 unaendelea. Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni katika mwaka 2019/20. Mwisho wa kumnukuu.

Kama wadau wa kusimamia, kufuatilia sheria na kanuni za usalama barabarani, tunawapa heko Serikali pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kukubali kuifanyia marekebisho sheria hii. Maeneo ambayo wadau wa usalama barabarani wanataka yafanyiwe marekebisho yapo ya aina mbili. Maeneo hayo ni moja, maeneo ya kipaumbele kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na pili, maeneo mengine ya jumla ndani ya sheria.

Katika maeneo ya kipaumbele kwenye mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani, yapo matano (5). Maeneo hayo ndiyo kipaumbele cha dunia kupitia Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na Umoja wa Mataifa kwa ujumla. Shirika la Afya limejikita katika kuhakikisha kuwa sheria za barabarani za nchi zinazokumbwa sana na ajali zinazingatia sana vihatarishi hivyo vikuu vitano. Na hii ni kutokana na taftiti mbalimbali zilizofanywa na kuonyesha kuwa maeneo hayo yakitiliwa mkazo siyo tu yanaweza kupunguza ajali bali pia kupunguza madhara



yanayotokea baada ya ajali. Katika vipaumbele hivyo, suala la kwanza ni udhibiti wa mwendokasi. Katika mabadiliko yatakayofanywa, iainishe kabisa maeneo maalumu ya spidi ya kilomita 50 kwa saa isiishie tu kusema ni maeneo ya makazi. Kwa sasa sheria katika kifungu cha 51(8) cha RTA haifafanui yapi haya ndiyo maeneo ya makazi, matokeo yake ni kuwa na tafsiri zinazotegemea utashi tu na hivyo kusababisha migogoro kati ya madereva na askari. Kwa kuwa makazi ya watu yamekuwa yakifuata barabara ipo haja ya kurekebisha sheria eneo hili ili ieleweke kabisa makazi yanaanzia nyumba ngapi au neno hilo linamaanisha nini hasa. Maeneo maalum yanayolengwa katika udhibiti zaidi wa spidi ni kama maeneo ya nyumba za ibada, shule, masoko na kadhalika. Na pia kwa magari ya yenye uzito wa chini ya Kilogram 3500 au tani 3.5 yanadhibitiwa kwenye ukomo wa mwendo wa kilomita 30 kwa saa na kilomita 50 kwa saa tu ila huko kwingine hayana ukomo, basi angalau sheria iwape nao ukomo.

Pili ni suala la ulevi. Kiwango cha ulevi kilichoainishwa na sheria kwa sasa katika kifungu cha 49 cha RTA, kinatakiwa kipungue kutoka 0.8g/dl(80mg) kwa kila 100ml (05g/dl) za damu ambacho ni kiwango cha kimataifa kwa dereva mzoefu na 0.2g/dl kwa kila 100ml (0.5g/dl) za damu kwa dereva mpya yaani, yule ambaye ndiyo kwanza anaanza kumiliki leseni na bado hajahuisha leseni yake.



Tatu ni suala la uvaaji wa kofia ngumu. Kifungu 39(12) kinalazimisha dereva wa pikipiki kuvaa kofia ngumu yeye na kuhakikisha abiria wake pia amevaa. Kifungu hiki hakimpi wajibu wa moja kwa moja abiria wa bodaboda kuvaa kofia ngumu, matokeo yake ni baadhi ya abiria kupanda pikipiki zisizo na kofia ngumu au zilizo na kofia ngumu moja au kupewa kofia ngumu. Mapendekezo yetu ni kuwa kila mmoja awajibike kwa kuvaa kofia ngumu. Abiria asiyevaa kofia ngumu aadhibiwe yeye abiria badala ya dereva.



Kipaumbele cha nne ni uvaaji wa mkanda. Kinapatikana katika kifungu 39(11). Sheria imlazimisha kila mtu anayekalia siti ya gari lazima aweamefunga mkanda na kama hajafunga aadibiwe yeye asiyefunga. Kwa sasa, sheria inamlazimisha abiria aliyekaa siti ya mbele tu na dereva kufunga mkanda. Lakini tumeona kabisa kuwa ajali ikitokea wanaoathirika sio abiria wa mbele tu, abiria wote kwenye gari wanaathirika sawasawa, hivyo ni muhimu abiria wote wavae mkanda.

Na tano ni kuhusu vizuizi vya watoto. Sheria itamke ulazima wa mtoto kukalishwa kwenye kiti chake maalumu awapo kwenye gari binafsi. Msisitizo tunauweka kwenye magari haya sababu tunajua wazi haya magari yanakimbia mno na sheria haiyapi ukomo wa mwendo kwenye maeneo yasiyo na ukomo wa mwendo, tofauti na magari makubwa ya kuanzia tani 3.5 na kuendelea ambayo yana ukomo wa mwendo wa kilomita 80 kwa saa.



Mabadiliko haya ndiyo tunataka kwa umoja wetu yafanyiwe marekebisho kisheria ili kuendana

na wakati wa sasa. Hali kadhalika suala lingine nyeti ni matumizi ya simu kwa madereva wakiwa barabarani. Kunatakiwa pia ifanyiwe kazi katika marekebisho hayo ili kupunguza ajali. Sheria inatakiwa kupiga marufuku matumizi ya simu kwa madereva wanapoendesha gari. Kwa mujibu wa mwanasheria wa TAWLA Mary Richard anasema, asasi yake kwa kushirikiana na asasi nyingine wanapigania kuwepo kwa sheria mpya ya usalama barabarani ambayo itapiga marufuku madereva kutumia simu wanapoendesha magari. Madereva hao wanapoendesha huku wakisikiliza simu, wapo hatarini kusababisha ajali. Idadi ya ajali zinazohusisha watumiaji wa simu ni nyingi na zinaweza kupungua pale sheria ya usalama barabarani itakataza matumizi ya simu kwa madereva wanapoendesha magari. Naye mwanaharakati wa usalama barabarani Augustus Fungo akinukuliwa kwenye mitandao alifafanua juu ya kasoro katika sheria ya usalama barabarani sura ya 168. Anasema sheria hiyo ya usalama barabarani wala kanuni zake haina kipengele chochote kinachopiga marufuku matumizi ya simu au kuweka hedifoni masikioni dereva anapoendesha gari au hata dereva kuangalia video ndani ya gari. Sababu ni kwamba, hii sheria ya usalama barabarani ni ya mwaka 1973. Licha ya kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara, marekebisho makubwa kabisa yalifanyika mwaka 1996 wakati huo ndiyo kwanza simu za mkononi zilianza kuingia nchini. Kanuni



za LATRA za usafirishaji abiria za mwaka 2007 kwa mujibu wa kanuni ya 18(1)(i) ni marufuku kwa dereva kuendesha gari huku akitumia simu. Hali kadhalika, kanuni ya leseni ya usafiriishaji magari ya mizigo ya mwaka 2012 kwa mujibu wa kanuni ya 28(1)(h) dereva amekatazwa kutumia simu au kifaa kinachofanana na hicho wakati wa kuendesha gari. Hivyo basi, tunaona kuwa kwa mujibu wa kanuni hizi za usafirishaji ni kosa kuendesha gari huku dereva anatomia simu. Iwapo kanuni za zamani zitaendelea kutumika basi ni kosa kwa dereva wa gari la mizigo na yule wa gari la abiria kuendesha gari huku akizungumza katika simu. Kutokana na sababu hii sheria mpya ihakikishe inaingiza katazo



la madereva kutumia simu wakati wakiendesha magari ili kupunguza vifo vinavyotokana na ajali za barabarani yaani marufuku itakuwa ni kwa dereva kushika simu kwa madhumuni ya kupiga, kupokea au kuandika ujumbe mfupi wa maneno wakati anaendesha gari.

Sanjari na kukubali kufanyia marekebisho sheria ya usalama, pia tunawapongeza kwa kupunguza ajali barabarani. Waziri Lugola anasema “katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 jumla ya matukio 2,593 yameripotiwa ikilinganishwa na matukio 4,180 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa vifo vitokanavyo na ajali za barabarani vimepungua kwa asilimia 38.7. Kupungua kwa ajali na vifo kumetokana na usimamizi mzuri wa Sheria za Usalama Barabarani; ushirikiano na wadau, sambamba na kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzingatia Sheria” mwisho wa kumnukuu. Kupungua ajali pia hutokana na matumizi sahihi ya barabara, chombo cha moto kinachotumika kuwa katika hali ya ubora na miundo mbinu na mazingira sahihi ya barabara, hivi vyote hutegemeana katika kupata usalama barabarani.

Wastani wa ajali 18,930 kwa mwaka ambayo pia ni wastani wa ajali 52 kwa siku. Uchunguzi uliofanywa umebaini kwamba, wastani wa watu 10 hufariki dunia kila siku nchini Tanzania kutokana na ajali hizo huenda zinasababishwa na vipaumbele hivyo tulivyoorodhesha hapo juu. Taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Jeshi la Polisi zinaeleza kwamba, mwaka 2013 ndio uliokuwa na ajali nyingi kutokana na kurekodi jumla ya ajali 24,480 ambapo kati ya hizo, ajali mbaya zilikuwa 3,545 ambazo zilisababisha vifo 4,091.

Kwa mujibu wa takwimu hizo makosa ya usalama barabarani yamekuwa yakiongezeka kwa kasi

kutoka makosa madogo 148,169 mwaka 2000 hadi kufikia makosa 1,381,705 mwaka 2015, likiwa ni ongezeko la mara tisa zaidi. Kuhusu ajali, nazo zimeonekana kupanda na kushuka kutoka 15,577 mwaka 2000 hadi 8,777 mwaka 2015 lakini ajali mbaya zilizosababisha vifo zimeongezeka kutoka 1,525 mwaka 2000 hadi 2,909 mwaka 2015. Aidha, idadi ya watu waliokufa kwenye ajali imeongezeka maradufu kutoka 1,812 mwaka 2000 hadi 3,574 huku idadi ya majeruhi ikipanda na kushuka kutoka 15,123 mwaka 2000 hadi 9,993 mwaka 2015., hata hivyo, taarifa kutoka ofisi za askari polisi idara ya trafiki zinaonyesha kuwa, mwaka 2014 vifo vilikuwa 3,760, majeruhi walikuwa 14,530 na ajali zilikuwa 14,360, mwaka 2015 vifo vilikuwa 3,468, majeruhi walikuwa 9,383 na ajali zilikuwa 8,337 na mwaka 2016 vifo vilikuwa 3,256, majeruhi walikuwa 8,958 na ajali zilikuwa 9,856. Pamoja na kupungua kwa idadi ya ajali, bado watu wengi wanapoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu, idadi ambayo ni kubwa ukilinganisha na nchi zilizoendelea au zinazodhibiti ajali.

Idadi ya vifo vinavyosababishwa na ajali za gari ni vingi, vinafukuzana na vifo vinavyotokana na malaria ambao ni ugonjwa unaoangamiza zaidi watoto wa chini ya miaka mitano. Tangu mwaka 2000 hadi 2015, jumla ya makosa madogo ya usalama barabarani yaliyoripotiwa yalikuwa 4,761,760, hivyo basi kupitia marekebisho ya kanuni na sheria za usalama barabarani zinaweka kupungua zaidi au kutoweka kabisa.

Mwalimu George Cleopa Mapunjo
+255 717 314 100

(Tunapokea habari zihusuzo Ajali za Barabarani jinsi zinavyo athiri familia na Taifa, tuma kwa tamwa@tamwa.org).

Sababu ya Sheria ya Usalama Barabarani kurekebisha bungeni

Na Mashauri Marwa

Utaratibu wa kupata ridhaa ya serikali kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 unaendelea. Muswada wa sheria hiyo utawasilishwa bungeni katika Mwaka 2019/ 2020."

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola analiambia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Aprili 24, 2019, wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yake kwa Mwaka 2019/2020.

"Katika Mwaka 2019/2020," Lugola anasema: "Jeshi (Polisi) litaendelea kusimamia sheria na kanuni za usalama barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali."

Mintarafu hali ya usalama barabarani nchini kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Machi 2019, anasema matukio 2,593 ya ajali yameripotiwa ikilinganishwa na matukio 4,180 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2017/ 2018. Vifo vitokanavyo na ajali za barabarani vimepungua kwa asilimia 38.7.

"Kupungua kwa ajali hizo kumetokana na usimamizi mzuri wa sheria za usalama barabarani, ushirikiano wa wadau, sambamba na kutoa elimu kwa jamii kuzingatia sheria," anasema.


Kabla ya kwenda mbali, niweke bayana pongezi zangu kwa serikali kwa jumla na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya ajali za barabarani kutokana na juhudi zao katika mchakato huu wa kuelekea kuifanya marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, hasa Sura ya 168 katika baadhi ya vipengele.

Hii ni kwa kuwa, sheria hiyo ina matundu mengi yanayosababisha Watanzania kupukutika kila kukicha kutokana na ajali za barabarani huku wengine wakipoteza mali, viungo vya miili yao na kupoteza uwezo kamili wa kufanya kazi za uzalishaji mali na ndiyo maana mchakato unafanywa ili irekebishwe kupitia chombo hicho chenye mamlaka ya kutunga na kurekebisha sheria.

UMUHIMU KUREKEBISHA SHERIA HII

Julai 2, mwaka jana wakati Rais John Magufuli anamwapisha ndugu Lugola kutumikia wadhifa wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi badala ya Mwigulu Nchemba wakiwa Ikulu Dar es Salaam, alisema: "nimekupeleka pale ukafanye kazi. Na wewe bahati nzuri ni askari..."

Rais anasema: "ajali za barabarani zimekuwa nyingi huku zikileta vifo, nimechoka kutuma rambirambi. Unatuma rambirambi hii kabla haijaisha nyingine inakuja napo unatakiwa kuandika. It's too much (imezidi), hakuna hatua zinazochukuliwa za kuwapa adhabu hata watu walioko kwenye maeneo hayo... Ninaposema nimechoka, maana yake nimechoka."



Taarifa ya WHO ya mwaka 2015 inaonesha kuwa, asilimia 76 ya ajali zinasababishwa na makosa ya kibinadamu wakati asilimia 16 zinatokana na ubovu wa vyombo vya moto. Asilimia 8 ni kutokana na miundombinu mibovu.



Kwa mujibu wa takwimu za Kikosi cha Usalama Barabarani, mwaka 2013 vifo vitokanavyo na ajali za barabarani Tanzania vilikuwa 4002, mwaka 2014 vilikuwa 3760, mwaka 2015 vifo vilikuwa 3468 na mwaka 2016 vilikuwa vifo 3256.

Taarifa ya mwaka 2018 ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonesha kuwa, takribani watu milioni 1.3 duniani hufariki kila mwaka kutokana na ajali za barabarani huku kati ya watu milioni 20 mpaka 50 wakipata ulemavu na wengi wao ni vijana.

WHO katika chapisho lake liitwalo: "Road Safety in the African Region 2015" la mwaka 2016 inasema kila siku, takribani vifo 650 hutoka katika barabara za Afrika. Linasema, licha ya Bara la Afrika kuwa na kiwango kidogo cha vyombo vya moto vya usafiri barabara (mfano magari) cha 46.6 (47) kwa kila watu 1000, Bara hili lina kiwango kikubwa cha vifo vya ajali barabarani cha watu 26.6 (27) kwa kila watu 100,000.

Kinyume chake, Bara la Ulaya lenye kiwango kikubwa cha magari cha 510.3 (511) kwa kila watu 1000, lina kiwango kidogo sana cha vifo vitokanavyo na ajali cha watu 9.3 (10) kwa kila watu 100,000.



Utafiti katika sehemu na nyakati tofauti unabainisha kuwa, sehemu kubwa ya vifo na madhara kutokana na ajali za barabarani hutoka katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania.

Kutokana na madhara ya ajali hizi kwa jamii na taifa kwa jumla, Mtandao wa Wadau Kutoka Asasi za Kiraia Unaotetea Marekebisho ya Sheria na Sera Ihusuyo Usalama Barabarani Tanzania, umekuwa ukiendesha mafunzo mbalimbali kwa wanahabari ili waunganishe nguvu kutoa elimu kwa umma mintarafu namna ya kuepuka ajali hizo na madhara yake.

Mtandao unapendekeza maboresho ya Sheria hii kwa mtazamo wa visababishi vikuu vitano yaani mwendokasi, viziwi kwa watoto (child restraints), uvaaji wa kofia ngumu (helmeti), uvaaji wa mikanda kwa abiria na ulevi/ unywaji pombe kwa madereva wanaoendesha gari.

Taasisi wadau wa mtandao huo ni pamoja na TAMWA, Chama cha wanasheria Tanzania (TLS), Mabalazi wa Usalama Barabarani (RSA), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (Shivyawata), Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), TCRF, Amend Tanzania, Taboa na Safe Speed Foundation.



Waziri Lugola anasema mchakato wa kupata ridhaa ya serikali ili mambo hayo yafikishwe na kujadiliwa na Bunge katika Mwaka 2019/ 2020 unaendelea.

Kimsingi, marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ni suala muhimu sana kwani sheria iliyopo inaonekana imepitwa na wakati, 'imetoboka na ina matundu mengi.'



Umuhimu wa Kofia Ngumu kuwa ya viwango

Umebainika kuwa asilimia kubwa ya kofia ngumu (helmet) zinazotumiwa na watumiaji wa usafiri wa pikipiki hapa nchini zimeingizwa kiholela huku pia hazikidhi ubora unaotakiwa na viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Utaratibu wa kuziingiza helmet nchini ni lazima kwanza zikishafika bandarini zikaguliwe na TBS ambapo inachukua kofia kadhaa kama sampuli na kwenda kuzipima kwenye maabara yake ili kubainisha kama zinaendana na ubora unaotakiwa ambao ni TZS 1478:2013.

Licha ya TBS kuwa kiwango hicho kinaelekeza malighafi za kutumika kwenye utengenezaji wa kofia hizo kwa kuzingatia ugumu wa gamba la kofia husika, uimara, ukubwa wa ndani wa kofia lakini zipo njia zisizo rasmi zinazotumiwa kuingiza kofia ngumu zisizokuwa na viwango.

Katika ufuatiliaji wa kina uliofanywa na TAMWA Konekt katika baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam, umebaini uwepo wa kofia zisizo na viwango ambazo kimsingi ndio zimeingizwa kwa njia hizo zisizosahihi.

Kofia hizo zinawahi kupasuka pindi zikipata msukosuko ambapo kama ikirushwa kutoka juu inapasuka haraka kutokana na utengenezwaji wake kuwa usio wa viwango ili hali inayokidhi viwango inapaswa kudunda na sio kupasuka.

TBS wanena

Akizungumza na gazeti hili Mkaguzi wa Ubora wa Bidhaa wa TBS, Yona Afrika alibainisha uwepo wa changamoto katika kukabiliana na

uingizwaji wa helmet feki nchini huku akigusia bandari bubu zinavyoshiriki katika hujuma hizo. Alitaja moja kati ya changamoto hizo ni ubadilishwaji wa mara kwa mara wa njia zinazotumika kuziingiza nchini kofia hizo ambapo maofisa wa TBS wanaweza kukaa bandari au mpaka mmoja kwa muda mrefu wakisubiri ziingizwe lakini waingizaji huwasiliana na kubadilisha njia.

Alisema kuwa hali hiyo imepelekea kuingizwa kwa kofia ngumu nyingi nchini na kuuzwa huku zikihatarisha usalama wa waendeshaji wa pikipiki hizo pamoja na abiria wake.

Alisema kwa upande wa TBS imekuwa ikiongeza umakini katika kuzikagua zile zinazopitia njia zinazotambulika ambapo pindi zikiingia nchini huchukua sampuli kadhaa na kisha kuyafunga kwa alama maalum makontena yenye mzigo husika na kuyaruhusu kuondolewa kwenye bandari husika kuepuka gharama ambazo wanaweza kutozwa.

Alisema, TBS ndani ya siku tatu hutoa majibu kama helmet walizokamata zinaendana na viwango vyao huku akibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 TBS iliziteketeza helmet zaidi ya 2,000 baada ya kubaini kutokuwa na ubora.

Alisema kiwango cha ubora za TBS kwa kofia ngumu cha 1478:2013 kimewekwa wazi wa wadau wote wanaoagiza bidhaa hizo na kuwa kwa wale ambao wanaziingiza tu nchini bila ya kuzingatia ndio wanaokumbana na adhabu husika.



Alibainisha kuwa kati ya adhabu ni kuwaambia warejeshe helmet hizo mahala walipozitoe au wazitekeze na kuwa hadi sasa kampuni 11 za hapa nchini ndio zinaagiza kofia za kiwango hicho.

Alisema kuwa TBS imeingia makubaliano na kampuni nne za kimataifa kufanya ukaguzi wa bidhaa zake zikiwamo helmet ambazo ni SGS, CCIS, Bureau Veritas na Intertek ambazo zimesambaa duniani kote na kati ya majukumu yake ni kufuatilia viwanda vinavyotengeneza helmet za kuja hapa nchini.

Alisema: "Ni kweli ipo mianya ambayo hutumiwa kuingiza nchini kofia ngumu hizo, na TBS inaendelea kukabiliana na hali hiyo na ndio maana kuna kofia nyingi feki mitaani, kazi

inaendelea kukagua na kuendelea kutoa elimu kwa wauzaji kuepuka kuuza kofia hizo.

Lakini pia wamiliki wa bodaboda wanapaswa kununua zile za kiwango kikubwa ambapo njia rahisi za wao kuzijua helmet bora ni kulinganisha utofauti wa bei zile zenye viwango bora zinazuzwa Shilingi 30,000 huku hizi nyingine ni hadi Shilingi 10,000 unapata".

Wasemavyo wadau wa helmet

Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Helmet Vaccine Initiative Tanzania, Alpherio Nchimbi anaishauri TBS kukagua na kuteketeza kofia ngumu feki zilizopo mitaani kama inavyofanya kwa bidhaa feki nyingine.

Anasema, kwa kuwa imethibitika kuwepo kwa kofia feki zisizokidhi viwango, kuna ulazima wa kuziteketeza huku akishangaa kutoona alama ya TBS katika helmet, alama inayodhihirisha kuwa ukaguzi wa ubora wa helmet hizo umefanyika.

Alisema "hata kwa zile ambazo zimeshakaguliwa ni vema basi kukawepo na alama ili mwananchi ajue kuwa helmet husika imekaguliwa, lakini pia ninashauri wawekezaji zaidi kujitokeza Taasisi yangu ipo tayari kushirikiana kiushauri na mwekezaji yoyote na pia uwekezaji wa bidhaa hiyo hapa nchini una fursa kubwa ya kibiashara".



Umuhimu wa kofia ngumu kwa matumizi ya chombo cha moto



Na Evance Ng'ingo

Kiama cha watumiaji wa usafiri wa pikipiki wasiozingatia kanuni za matumizi ya kofia ngumu(helmet) kimekaribia kwa kuwa muswada wa mabadiliko ya sheria ya Usalama Barabarani ya 1973 unatarajiwa kutinga bungeni septemba hii.

Usafiri wa bodaboda ni moja kati ya njia za usafiri zinazotumiwa zaidi katika mazingira ya mijini na vijijini, lakini unakabiliwa na changamoto ya uhakika wa usalama wake hali iliyosababisha wadau wa usalama barabarani kusisitiza matumizi sahihi ya kofia ngumu ili kuwakinga watumiaji kupatwa na majeraha pindi ajali ikitokea.

TAMWA Konnect limefanya ufuatiliaji kwenye mwongozo wa Sheria ya Usalama Barabarani na kubaini mapungufu kwenye sheria hiyo ya mwaka 1973. Katika kifungu cha 39(12) cha Sheria ya Usalama Barabarani, 1973 kimentaja dereva wa pikipiki kuwa ndiye anayepaswa kuvaa *helmet* lakini abiria hajatajwa kama na yeye anapaswa kuvaa *helmet*.

Hayo ni kati ya mapungufu kwenye sheria hiyo ya 1973 katika kuhakikisha usalama kwa abiria unakuwepo, hivyo wadau wa usalama barabarani kwa muda mrefu wameanzisha mchakato huo wa mabadiliko ya sheria kwa kupendekeza sheria kadhaa mpya na nyingine kufanyiwa marekebisho ambapo ya matumizi ya *helmet* ni kati ya zinazotajwa kupendekeza kufanyiwa marekebisho.

Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama barabarani, ASP Deus Sokoni ameliambia gazeti hili kuwa hadi sasa mchakato wa mabadiliko ya sheria hayo umefikia mahala pazuri na kuna kila dalili kuwa Septemba mswada utajadiliwa bungeni.

Congratulations to Ministry of Home Affairs on Road Safety Amendments Process



Group photo on 28th June, 2019 at the TAMWA Conference Hall during the training on how to report Road Safety news for the tradition media journalists whereby the Acting Director for Information Rodney Mbuya (With Black Suit) at the middle from the Ministry of Information, Youth, Culture and Sports officiated the training. The training funded by the Global Road Safety Partnership under the Bloomberg Philanthropies Fund.

The Government that works on progressive ways always listens to what citizens wants and work on it on time. That means so many noises at the community on the amendment of Road Traffic Act (RTA) of 1973, that have been done by the different stakeholders requires cases related to road crashes to be historical issues in Tanzania.

According to the Minister for Home Affairs (MOHA) Hon. Kangi Lugola (MP), on his Speech Budget Presentation at the 2019 session at the National Parliament; he was quoted "Honorable National Assembly Speaker, on the year 2019/2020, Police will continue to work on supervising security at the country including road safety in collaboration with other stakeholders. At the same time, all plans to fulfill proposals to amend the RTA section/chapter 168 shall be done and the manuscript shall be presented at the Parliament by this 2019/20" ...end of the quotation.

Helmet Uses

It was known that about 80% of the helmets that are in the market and used by most of Motorcycle drivers entered at the market areas unlawful and they are not meeting the actual and proper standard that is required by the Tanzania Bureau of Standard (TBS).

Alisema kuwa kipengele cha matumizi ya *helmet* kwenye sheria hiyo ni kati ya maeneo yenye mapungufu ambayo yamesahauliwa kufanyiwa mabadiliko kwa kuwa kwa sasa sheria hiyo ya 1973 haiendani kabisa na uhitaji wa sasa wa usafiri huo.

Alisema kwa sasa usafiri huo unatumiwa kama moja kati ya njia kuu za usafiri hapa nchini na umekuwa ukitumiwa na watu wa mijini na vijijini na hivyo matumizi ya *helmet* kwa abiria ni lazima na kuwa wameshauri adhabu kali kwa watu watakaokamatwa hawajavaa kofia hizo.

Alisema, mapendekezo ya wadau ni kuwa sheria ielekeze kuwa abira naye anapaswa kuvalia kofia ngumu wakati wote atumiapo usafiri huo kama ilivyo kwa dereva na pia wamependekeza adhabu kali kwa watakaokamatwa kutovaa kofia hizo.

Alisema, "wadau wa usalama barabarani hatulali tunataka kuhakikisha kuwa sheria hiyo ya mwaka 1973 inafanyiwa marekebisha ambapo sio tu katika matumizi ya *helmet* ila kuna mambo mengine kadhaa kama vile, matumizi ya mikanda, kiwango cha kilevi kwa dereva, matumizi ya viti maalum vya kubebea watoto wadogo kwenye usafiri na mengineo mengi"

Kwa kuwa habari hii limejikita zaidi katika kufuatilia matumizi ya helmet, limefanya ufuatiliaji kubainisha waendesha pikipiki na abira wanaokamatwa kwa kutovaa *helmet* na kutozwa faini ya Shilingi 30,000 wanabanwa na sheria gani ambapo limebainisha kuwa ni Kanuni ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Ardhi (LATRA) ndio inayotoa mwongozo huo.

Gazeti limebainisha kuwa hata hivyo kanuni hiyo zimewabana wanaotumia pikipiki kibiashara ndio dereva wake na abiria wanabanwa kuvaa helmet, lakini wanaotumia usafiri huo kwa matumizi binafsi kanuni hiyo haiwabani.

Mwandishi wetu alizungumza na Mwanasheria John Mwakibete ambaye anaeleza kuwa kuna umuhimu zaidi wa matumizi ya sheria katika kutoa mwongozo wa matumizi ya helmet ikilinganishwa na mwongozo huo kutolewa kwenye kanuni.

Aligusia kuwa licha ya kuwa serikali chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani (Ministry of Home Affairs-MoHA), kwa kushirikiana na wadau wa sekta husika inaweza kutunga na kuidhinisha kanuni kutumika katika kukidhi matakwa ya suala husika lakini suala hilo likitungiwa sheria linaweza kuwa na uzito stahiki.

Alifafanua kuwa kama iwapo mwendesha boda boda au abiria akikamatwa na kuamrisha kulipa faini ilivyoelekezwa na kanuni iwapo akikataa au kushindwa kulipa na kupelekwa mahakamani, mahakama inaweza kuangalia sheria mama inaelekeza nini na iwapo ikikuta hakuna kipengele cha kumbana abiria kama ilivyo hiyo ya 1973 abiria huyo anaweza kuachiwa huru hasa kama kanuni ikiwa haitoi mwongozo wa adhabu kwa kosa husika.

Alisema, "kuna haja ya sheria kusema wazi kuhusiana na hilo na sio tu kanuni peke yake licha ya kuwa kanuni inatoa mwongozo ambao unaweza kukubalika na kutumiwa kama sheria kabisa mahakamani katika kubana baadhi ya vitu ila pia inakuwa na nguvu zaidi kama sheria yenyewe mama ikiweka wazi kuhusiana na suala hilo".

TBS clarified these, according to their system, they are required to make the spot checking on the all products that arrive by ships or airplanes, this including helmets products, and all products that comes from outside the country must be tested its efficiency as per international measurement standards which is known (TZS 1478:2013).

TBS also clarified that; proper helmet has to be made by proper materials that can support the best standards and durability of the required helmet. Substandard helmets have been circulated by black markets. Therefore, the required strong law that can mention the standard of helmet is really required to prevent our people from the bad head on collision that happened to the people and mostly the young ones.



Traffic Police explain to a Motorcycle driver the importance of helmet to his safety, this picture taken recently at the city of Dar es Salaam.

Reasons for Road Safety Law amendment stated at the Parliament.

"A process to get an official approval for the Road Traffic Act of 1973 amendment on the Chapter 168 is still going on. And the amendment shall be submitted at the parliament within this year 2019/20.

The Home Affairs Minister, Kangi Lugola (MP), briefed the Members of Parliament at the Parliament session on April 24th, 2019 as he was presented the income and expenditure Budget of his Ministry for the year 2019/20. He also agreed to work seriously to make sure that, Tanzanian Police will work properly on Road Safety issues in collaboration with other stakeholders.



President of the Union Republic of Tanzania Honorable John Pombe Magufuli, in a group photo with Traffic Police of Tanzania recently.

A milestone achievement in road safety journey

By Crispin Gerald

“We can prevent millions of road traffic fatalities and injuries through stronger laws, more effective enforcement and better infrastructure,” said Michael R. Bloomberg founder of Bloomberg Philanthropies Initiative for Global Road Safety.

The statement reflects the fact that, road crashes that according to World Health Organization (WHO) Global status report on road safety 2018 said to have contribute to 1.35 million traffic deaths, but it can be preventable and eliminated.

The report stated that road traffic injuries is the 8th leading cause of death (silent killer), for all age groups, up from the 9th leading cause of death 10.

